

## **Ilani ya Kutoruhusu Ubaguzi**

Mfumo wa afya wa Hospitali ya Concord unazingatia sheria zinazotumika za haki za kiraia za Serikali kuu na za Jimbo. Sera zetu zimepiga marufuku ubaguzi (ikiwemo tofauti isiyo ya haki katika matibabu, unyanyasaji, udhalilishaji, au uonevu) dhidi ya mtu ye yeyote kwa misingi ya mbari, rangi, kabilia, asili, asili ya kitaifa, umri, hali ya ndoa, hali ya kijamii na kiuchumi, lugha, ulemavu wa kimwili au kiakili, jinsia (ikiwemo sifa za kijinsia na uhuntha, ujauzito au hali zinazohusiana, mwelekeo wa kijinsia wa kweli au unaodhaniwa, utambulisho wa kijinsia au mwonekano kijinsia, na dhana za kijinsia) au hali nyingine yoyote inayolindwa kama ilivyobainishwa na sheria za Serikali kuu, jimbo au za mitaa.

Mfumo wa afya wa Hospitali ya Concord pia unatoa huduma kama vile:

- Wakalimani wa lugha ya ishara waliohitimu bila malipo ili kuwasaidia watu kuwasiliana kwa ufanisi inapohitajika.
- Taarifa zilizoandikwa katika miundo mingine (herufi kubwa, miundo ya kielektroniki inayoweza kufikiwa).
- Huduma za usaidizi wa lugha bila malipo kama vile wakalimani waliohitimu na taarifa zilizoandikwa kwa lugha nyingine kwa watu ambao lugha yao kuu si Kiingereza.
- Marekebisho au mabadiliko yanayofaa katika sera, mazoea, na taratibuzetu kwa misingi ya ulemavu, isipokuwa kama yatasababisha ugumu usiofaa au mabadiliko makubwa ya mpango.
- Huduma za usaidizi kwa misingi ya imani za kidini zinazoshikiliwa kwa dhati ambazo hazisababishi mzigo mkubwa.

Ikiwa unahitaji huduma za usaidizi, mabadiliko, usaidizi na huduma za ziada zinazofaa, au huduma za usaidizi wa lugha, tafadhalii wasiliana na (603) 415-6602, bila malipo (800) 327-0464, kiendelezi 6602, TTY (603) 227-7033 au VP (603) 565-4660 na uombe Programu ya Huduma za Lugha na Ufikiaji.

Ikiwa wewe au mwakilishi wako mnaamini kuwa mfumo wa afya wa Hospitali ya Concord ulikubagua au ulishindwa kutoa huduma hizi kwa misingi ya ubaguzi, wewe au mwakilishi wako mnaweza kuwasiliana na Mratibu wa Haki za Kiraia, kwa: Mkurugenzi wa Uzingatiaji, 250 Pleasant St. Concord, NH 03301, 603-789-9104, TTY: (603) 228-7135, Faksi: (603) 227-7586, au [civilrightscoordinator@crhc.org](mailto:civilrightscoordinator@crhc.org). Unaweza kuwasilisha malalamiko ana kwa ana au kwa barua, faksi, au barua pepe. Ikiwa unahitaji usaidizi wa kuwasilisha malalamiko, Mkurugenzi wa Uzingatiaji wa mfumo wa afya wa Hospitali ya Concord yupo tayari kukusaidia.

Pia unaweza kuwasilisha malalamiko ya haki za kiraia na Mashirika yafuatayo ya Serikali kuu:

- U.S. Department of Health and Human Services  
200 Independence Avenue, SW Room 509F, HHH Building  
Washington, D.C. 20201  
1-800-368-1019, 800-537-7697 (TDD)  
Fomu za kuwasilisha malalamiko zinapatikana kwenye  
<https://www.hhs.gov/ocr/complaints/index.html>

- U.S. Commission on Civil Rights  
1331 Pennsylvania Avenue, NW  
Washington, DC 20425  
Simu: 1-202-376-8128, Huduma ya TTY ya kubadli maandishi kuwa Sauti: 711  
Tovuti: <https://www.usccr.gov/contact/complaints>

Ilani hii inapatikana kwenye tovuti ya mfumo wa afya wa Hospitali ya Concord kwenye  
<https://www.concordhospital.org/nondiscrimination-notice/>